

KILOMBERO VALLEY TEAK COMPANY LIMITED  
**SERA YA MAHUSIANO NA JAMII**

TOLEO LA JUNI, 2024



## Utangulizi

KVTC inatambua kuwa inafanya kazi kwenye bonde la Kilombero ili kuimarisha ubora wa maisha ya wadau wote. Kampuni itahakikisha kuwa wadau wa ndani wanashughulikiwa katika namna sawa kama wadau wengine. Kampuni itafuata sera ambazo zinahamasisha utambuzi wa faida muhimu za bonde la Kilombero. Kampuni itajitahidi kuhakikisha kuwa jamii hazipati hasara kutokana na shughuli za kampuni.

## Sera

1. KVTC itachukua nafasi ya ujirani mwema kwa jamii.
  - a. Kampuni itakuwa na mawasiliano ya mara kwa mara na jumuiya za jirani.
  - b. Kampuni itazisaidia jamii katika maendeleo yao kwa kushauriana jumuiya za jirani.
  - c. Kampuni itakubali mahali sahihi pa mipaka yake na jumuiya za jirani.
  - d. Kampuni itaruhusu Bidhaa za Msitu ambazo si za mbao kutumiwa na jamii pindi inapoweza kuonyeshwa kuwa endelevu na kudhibitiwa vya kutosha.
2. KVTC itaanzisha uelewa wa kina wa jamii na mahitaji yao.
  - a. Kampuni itafanya tathmini ya athari ya kijamii ya mazingira ya shughuli zake.
  - b. Kutakuwa na mchakato kuhakikisha kuwa tathmini hii ya athari ya kijamii inapitiwa mara kwa mara.
  - c. Maeneo ya kiutamaduni, kidini na kihistoria yatabainishwa kwa kujadiliana na jamii na taratibu za kuhakikisha ufikiaji na kuyalinda zitaanzishwa wakati wa uendeshaji wa msitu.
  - d. Kampuni itazingatia kikamlifu haki zote za binadamu kwa wadau wake wote kama ilivyoainishwa katika katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
3. Kampuni itaheshimu haki za kawaida za jamii na kuandaa taratibu ili kuhakikisha kuwa migogoro kuhusiana na haki za kawaida inashughulikiwa kwa namna inayojulikana na pande zote.
  - a. Utaratibu wa kusuluhiha mgogoro utakubaliwa na jamii kabla ya kutokea kwa mgogoro.
  - b. Pindi mgogoro ukitokea hakuna shughuli za msituni zitakazofanywa kwenye eneo la mgogoro bila ya makubaliano na jumuiya ilioathiriwa.
4. Kampuni itazifidia jamii kwa uharibifu wowote usio wa uangalifu uliosababishwa kwenye vyanzo vyao vya kawaida au haki katika Kitengo cha Usimamizi wa Msitu.
  - a. Kutakuwa na utaratibu wa kuamua fidia itakayokubaliwa na jamii.
5. KVTC itajitahidi kuimarisha uchumi wa ndani.
  - a. Kampuni itatoa kipaumbele kwa wafanyakazi wa ndani (maeneo ambayo kampuni inafanya kazi) kwa nafasi zote, ambazo wana sifa.
  - b. Kampuni itatoa huduma na usambazaji wake kadiri iwezekanavyo ndani.
  - c. Kampuni itatoa sehemu ya uzalishaji wake kwa wajasiriamali wa ndani kwa ajili ya uchakataji wa ndani.

Irvine Kanyemba Mkurugenzi Mtendaji